...Tanzania (TRA) wakati walipomtembelea ofisini kwake jana, kuhusu kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea.

# Benki ya Kilimo yatoa mkopo kiwanda cha Maziwa

**Na ELIZABETH KILINDI - NJOMBE**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imetoa mkopo wa zaidi ya Sh milioni 600 kwa kiwanda cha kuchakata maziwa Njombe kwa ajili ya kusaidia kuendeleza uzalishaji wa maziwa pamoja na kulipa kulipa madeni ya wafugaji waliokuwa wanakidai kiwanda hicho.

Makabidhiano ya kupokea mfano wa hundi ya fedha yamefanyika juzi kiwandani hapo mbele ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Uwekezaji, Angellah Kairuki, ambapo alitoa rai kwa Watanzania kubobea katika elimu ya usindikaji wa maziwa viwandani baada ya kubainika kuwepo na changamoto ya wataalamu wenye ujuzi sasa ni wachache nchini.

Alisema Tanzania kwa sasa ina wataalam hao watatu pekee wenye ngazi ya elimu ya juu mmoja akiwa ni meneja wa kiwanda hicho cha Njombe Milik Factory, huku wawili wakiwa nchi za Uganda na Kenya.

"Nafahamu Wizara ya Mifugo wameshaanza mashauriano na wizara ya elimu kuona ni namna gani tunaweza kutoa pia kozi ya namna hii kwa kiwango cha digrii hapa hapa nchini, hivyo ni hamasishe vijana wengine kuona umuhimu wa fani hii na waweze kujiunga na kozi hiyo ili waweze kuwa wabobezi wa sekta ndogo ya usindikaji maziwa,"alisema Kairuki.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Biashara na Mikopo wa Benki ya TADB, Wende Mengele alisema wametoa mkopo kwenye kiwanda hicho ikiwa ni awamu ya pili ili kusaidia kiwanda kujiendesha na kukabiliana na changamoto ambazo zilikuwa zikikwamisha kuongeza uzalishaji wa maziwa kwenda sokoni.

"Hii hela ambayo imetoka milioni 696 inaenda kwa ajili ya kuhakikisha maboresho ya ndani ya kiwanda, kuna vitu vingi sana ambavyo vimekufa vya maabara,majokofu na vilevile kuwalipa wakulima na wafugaji ambao wanakidai kiwanda," alisema Wende.

Meneja wa kiwanda hicho, Shaibu Kassim alisema kupatiwa mkopo huo kutawafanya wakimbie baada ya serikali kufanya mabadiliko makubwa ndani ya kiwanda ikiwemo kubadilisha mfumo wa kiuongozi.

"Tangu nimekuja tumepunguza kiasi kikubwa sana cha madeni ambayo kiwanda kilikuwa kinadaiwa na wafugaji wanaounda ushirika, tumelipa fedha nyingi sana kiasi kisichopungua Shilingi milioni 180 kwa miezi mitatu, tuna amani mkopo huu utakuwa ni msaada na tija kwetu sisi kiwanda," alisema Kassim.

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Katarina Revocati alisema kutolewa kwa mkopo kwenye kiwanda hicho ni mkakati wa serikali kuendelea kukifanyia maboresho kiwanda hicho ili kiongeze uzalishaji wa maziwa mkoani Njombe.

"Wito wangu kwa wafugaji wa Njombe waendelee kujitahidi kulisha mifugo vizuri maziwa yazalishwe kwa wingi kwa sababu kiwanda kinaenda kufanya kazi kubwa, uwezo wa kiwanda unaenda kuimalishwa sana hivi sasa," alisema Katarina.

Scanned with CamScanner





# ...na ...ila

kushirikiana
utoka Njombe,
valisema kama
na hasira katika
tokea tatizo ni
vazee na kukaa
tatizo
wake Chifu
hehe Mkoani
api Mkwawa
gumza mara
nikwa alitoa
chi wa mkoa
mila na
ila hilo huku
imani na umoja
a uchaguzi.
CCM Mkoa wa
Pinda, alisema
licha ya elimu
mdogo alionao
uchifu.
wa jukumu la
dumisha mila
o hatupaswi
abu za msingi
shima kubwa
m licha ya umri
'alisema Pinda.

# Kiwanda cha maziwa chapatiwa mkopo

**Njombe**
**NA MICHAEL KATONA**

KIWANDA cha kuchakata maziwa cha Njombe Milk Factory cha mkoani hapa kimepatiwa mkopo wenye zaidi ya sh. milioni 696 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa ajili ya kusaidia kuendeleza uzalishaji wa maziwa pamoja na kulipa kulipa madeni ya wafugaji.

Makabidhiano ya kupokea mfano wa hundi ya fedha kiasi cha zaidi ya sh. milioni 696 yamefanyika mbele ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Uwezeshaji, Angelah Kairuki, ambaye ametoa rai kwa Watanzania kubobea katika elimu ya usindikaji wa maziwa viwandani.

Alisema Tanzania kwa sasa ina wataalam watatu pekee wenye ngazi ya elimu ya juu mmoja akiwa ni meneja wa kiwanda hicho huku wawili wakiwa nchi za Uganda na Kenya.

"Nafahamu Wizara ya Mifugo wameshaanza mashauriano na Wizara ya Elimu kuona ni namna gani tunaweza kutoa pia kozi ya namna hii kwa kiwango cha degree hapa hapa nchini, hivyo ni hamasishe vijana wengine kuona umuhimu wa fani hii na waweze kujiunga na kozi hii ili waweze kuwa wabobezi wa sekta ndogo ya usindikaji maziwa," alisema Kairuki.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Biashara na Mikopo wa Benki ya TADB, Wende Mengele, alisema wametoa mkopo kwenye kiwanda hicho ikiwa ni awamu ya pili ili kusaidia kiwanda kujiendesha na kukabiliana na changamoto ambazo zilikuwa zikikwamisha kuongeza uzalishaji wa maziwa kwenda sokoni.

"Hii fedha ambayo imetoka sh. milioni 696 inaenda kwa ajili ya kuhakikisha maboresho ya ndani ya kiwanda, kuna vitu vingi ambavyo vimekufa vya maabara, majokofu na vilevile kuwalipa wakulima na wafugaji ambao wanakidai kiwanda," alisema Wende.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Katarina Revocati, alisema kutolewa kwa mkopo kwenye kiwanda hicho ni mkakati wa serikali kuendelea kukifanyia maboresho kiwanda hicho ili kiongeze uzalishaji wa maziwa mkoani Njombe.

# ...ASS yawafikia wajasiriamali wengi

# Kutoa elimu juu ya kanuni za ufugaji bora na wenye tija katika kata zote

Jedwali: Hali ya Utekelezaji wa malengo kwa mazao makuu.

| Na | UTEKELEZAJI HALISI MSIMU WA KILIMO 2017/2018 | | MALENGO YALIYOWEKWA KWA MSIMU 2018/2019 | |
|---|---|---|---|---|
| Zao | (Ha) | (Tani) | (Ha) | (Tani) |
| Mahindi | 42,494.3 | 84,988.6 | 45300 | 90600 |
| Mtama | 7,863 | 9,828.98 | 12540 | 15048 |
| Uwele | 11,835 | 11,835 | 9540 | 11448 |
| Mpunga | 51 | 153 | 100 | 300 |
| Jumla | 62,192.3 | 106,652.58 | 67530 | 117283.5 |
| Ufuta | 5,430.2 | 4,344.2 | 9520 | 9520 |
| Alizeti | 25,071.98 | 20,057.6 | 28230 | 33876 |
| Karanga | 2,170.94 | 868.4 | 3500 | 2800 |
| Pamba | - | - | 2000 | 4000 |
| Jumla | 32,673.12 | 25,270.2 | 43250 | 50196 |
| Kunde | 131 | 52.4 | 450 | 360 |
| Mbaazi | 6,047 | 2,418.8 | 4200 | 3360 |
| Dengu | 250 | 300 | 350 | 525 |
| Njugu mawe | 412 | 164.8 | 150 | 90 |
| Jumla | 6840 | 2,936 | 5150 | 4335 |
| Muhogo | 1803 | 782.7 | 9240 | 92400 |
| Viazi vitamu | 978 | 606 | 3200 | 12800 |
| JUMLA | 2781 | 1388.7 | 14,475 | 123,108 |

na kutounganishwa na umeme wa TANESCO wenye gharama ya 183,000,000 ambayo kwa sasa Halmashauri haina fedha hiyo na inafanya jitihada za kuomba kwa wafadhili wakiwepo 'LIC'.

Skimu hii imeweka mtandao wa umwagiliaji katika hekta 30 za umwagiliaji kwa matone, kati ya hekta 30 za awamu ya kwanza hekta 2.5 zimetengwa kwa ajili ya vijana na hekta 2.5 zimetengwa kwa ajili ya akina mama.

Mradi huu hadi kukamilika kwake utagharimu sh. milioni 811,000,000,000. Hivi sasa mradi wa kidoka una changamoto ya umeme ambapo gharama za uwekaji umeme zilizowasilishwa na TANESCO ni sh. milioni 183,000,000.

Umeme ukipatikana mradi huo unaotarajiwa kuwa wa manufaa makubwa kwa vijana utaanza kutekelezwa.

Pamoja na kuwa na eneo dogo linalomwagiliwa, Wilaya ya Chemba ina eneo kubwa linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mabonde ya Ndoroboni, Babayu na Jogolo yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 3,000 kwa kutumia uvunaji wa maji ya mvua.

**UFUGAJI**

Halmashauri ya Wilaya ina Jumla ya ng'ombe, 297,073, mbuzi 209,673, kondoo 98,304, nguruwe 600, kuku 352,000, bata 120,000, punda 12,933, mbwa 3,081, paka 600 na sungura 5,400.

Lengo la sekta ya mifugo ni kusimamia ufugaji wenye tija kwa kutoa elimu ya ufugaji bora kwa nia ya kuboresha afya ya mifugo na kuongeza uzalishaji na mazao yake kama nyama, maziwa na mayai bila kuathiri mazingira.

**MAMBO YAFUATAYO YAMETEKELEZWA:-**

Kutoa elimu juu ya kanuni za ufugaji bora na wenye tija katika kata zote.

Kutoa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu kwa ng'ombe na mbuzi katika kata zote 26, ambapo ng'ombe 135,478 na mbuzi 38,226 wamechanjwa na Jumla ya Tsh. 154,875,000/= zimekusanywa.

Kufuatia agizo la kupiga chapa mifugo, katika Halmashauri yetu Jumla ya ng'ombe 259,726, punda 852 sawa na asilimia 99 ambapo Jumla ya Tsh 128,798,000/=.

Tumefanikiwa kuanzisha vikundi mbalimbali vya ufugaji vipatavyo 41 vya ufugaji kuku na mbuzi.

Kutoa chanjo dhidi ya ugonjwa wa kideri kwa kuku ambapo jumla ya kuku 186,783 katika kipindi cha Julai 2018 hadi January 2019.

Kukinga mifugo dhidi ya magonjwa yatokanayo na kupe kwa kuogesha mifugo ambapo idadi ya mifugo iliyoogeshwa mpaka sasa ni ng'ombe 107,251 na mbuzi/kondoo 69,531 kwa kipindi cha Julai 2018 hadi January 2019.

Kusimamia uboreshaji/ujenzi wa miundombinu katika mnada wa mifugo Magambua unaofadhiliwa na LIC ambao hadi kukamilika unakadiriwa kugharimu Jumla ya Tsh. 63,904,000/= ambapo kati ya hizo Tsh. 9,000,000/= ni mchango wa Halmashauri.

Kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha wafugaji na wananchi kutenga maeneo ya malisho katika kata zote 26 na vijiji 114 na kuyaendeleza maeneo yatakayotengwa kwa kuzalisha vyakula vya mifugo.

Kuunda umoja wa Chama cha Wafugaji kuanzia ngazi ya kijiji na kata na uchaguzi kwa ngazi ya Wilaya umefanyika Tarehe 23.2.2019 na kupata uongozi wa Chama hicho.

**NISHATI YA UMEME**

Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa umeme wilayani Chemba bado siyo ya kuridhisha kwa kuwa Vijiji vingi na hata Makao Makuu ya Wilaya kutosambaziwa umeme ingawa katika maeneo kidogo yenye umeme mgao kwa kipindi kirefu sasa umetoweka.

Idadi ya vijiji vyenye umeme ni 31 sawa na asilimia 27. 2 ya vijiji vyote 114. Usambazaji wa umeme kupitia Mradi wa REA III (awamu ya kwanza).

Vijiji 27 vinatarajiwa kupatiwa huduma ya umeme na kufanya jumla ya vijiji 58 sawa na asilimia 50.9 kuwa na huduma ya umeme.

Aidha, vijiji 56 vilivyo baki vinatarajiwa kupatiwa huduma ya umeme kupita REA III (awamu ya pili) na hivyo kukamilisha azma ya Serikali ya awamu ya Tano ya kuvipatia vijiji vyote 114 umeme ifikapo mwaka 2020.


Aidha, Shirika la Umeme (TANESCO) linaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma bora ya umeme kwa kuanzisha ofisi ya Wilaya na kuendelea kufanya ukarabati wa miundombinu kila inapopata hitilafu.



Bwawa la Maji katika Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji-Kidoka

# TADB provides 700m/- to Njombe milk factory

By DAILY NEWS Reporter



TANZANIA Agricultural Development Bank (TADB) has provided 696m/-loan to Njombe Milk Factory to support a revival programme of the milk processing plant in Njombe Region. The Minister of State in the Prime Minister's Office (Investment), Ms Angela Kairuki, presented a dummy cheque of the amount on Wednesday to Njombe District Commissioner (DC), Ruth Msafiri to launch additional rescue package of the milk processing factory.

Commenting, the Minister commended the bank for its continued support in facilitating payments to farmers, rehabilitating the factory's infrastructure and managerial assistance. Ms Kairuki urged the bank to continue supporting the factory to ensure that it reaches its full capacity utilisation of 20,000 litres per day from the current 3,000 litres.

On her part, TADB's Acting Director of Credit and Business, Wende Mengele, said farmers should be assured that TADB is committed to supporting them.

She said the Njombe Milk Factory project was on a growth trajectory would soon start paying dividends to its shareholders.

Ms Mengele urged the management of the factory to work diligently to develop and roll out new products, which will easily be sold to the market given Njombe's strategic advantage of serving Lindi, Mtwara, Ruvuma regions and regional markets of Malawi and Mozambique.

The main shareholders of Njombe Milk Factory are Njombe Livestock Farmers Organization (NJOLIFA), which owns 20 per cent shares, Njombe Local Government Authority 19 per cent stake and the Roman Catholic Njombe 9.7per cent.

Scanned with CamScanner